# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 055
MEI 2025

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY



## 1 SULUHU MGAWANYO WA MAPATO WA HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA NCHINI YAPATIKANA

## 2 VIONGOZI NA WATAALAMU WA HALI YA HEWA WA ZIMBABWE WAFANYA ZIARA YA MAFUNZO YA SIKU TANO NCHINI TANZANIA



## 3 FAHAMU ZAIDI:
## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2025



KITAIFA

# SULUHU MGAWANYO WA MAPATO WA HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA NCHINI YAPATIKANA

**Dar es Salaam**




Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) pamoja na Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) wafanikisha upatikanaji wa suluhu ya mgawanyo wa mapato yatokanayo na huduma za usafiri wa anga nchini.

Suluhu hiyo ilipatikana kupitia kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano ya pamoja baina ya wakuu wa taasisi hizo katika ukumbi wa mikutano wa TAA uliopo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, tarehe 23 Mei 2025.

Mkataba huo unafuatia kuundwa kwa mfumo wa kielektroniki (Ankara Jumuishi) utakaosaidia kuimarisha uwazi, ufanisi na tija katika mgawanyo wa mapato yatakayokuwa yamekusanywa kwa kuingizwa moja kwa moja kwenye taasisi husika kulingana na asilimia zilizokubalika. Mfumo unatarajiwa kuanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai 2025.

Wakizungumza katika zoezi la utiaji saini, Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Bw. Abdul Mombokaleo alieleza kuwa mfumo huo wa kielektroniki utarahisisha mgawanyo wa mapato na kuwezesha kila taasisi kupata mgao wake kwa wakati ili kusukuma gurudumu la maendeleo ya nchi yetu. Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC), Dkt. Ladislaus Chang'a aliwashukuru viongozi wenzake kwa kufanikisha kukamilika kwa mfumo huo na kusisitiza kuwa mfumo huo utachangia sana kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kwa kupunguza muda na nguvu kubwa iliyokuwa inatumika kufuatilia mapato yatokanayo na huduma zitolewazo na kila taasisi.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Mhandisi Peter Ulanga alipongeza muitikio kutoka pande zote wa kutekeleza maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya mifumo ya taasisi za serikali kusomana, naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Bw. Daniel Malanga alipongeza hatua iliyofikiwa sababu itaboresha utoaji huduma ndani ya viwanja vya ndege nchini.





## KIMATAIFA

# VIONGOZI NA WATAALAMU WA HALI YA HEWA WA ZIMBABWE WAANZA ZIARA YA MAFUNZO YA SIKU TANO NCHINI TANZANIA

**Dar es Salaam**



Viongozi waandamizi na wataalamu wa Idara ya Hali ya Hewa Zimbabwe (Meteorological Services Department (MSD)) walianza ziara ya mafunzo ya siku tano nchini Tanzania kuanzia tarehe 19 hadi 23 Mei 2025 ili kujifunza na kujenga uwezo na umahiri katika masuala mbalimbali ya hali ya hewa katika ofisi za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) zilizopo Ubungo Plaza, Dar Es Salaam, nchini Tanzania.

Akiwasilisha salamu za ukaribisho, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, na Makamu Mwenyekiti wa IPCC, Dkt. Ladislaus Chang'a aliushukuru uongozi wa MSD Zimbabwe kwa kuichagua TMA nchini Tanzania kati ya nchi zote Afrika ili kuja kufanya ziara ya mafunzo kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika taasisi yao.



‘Ni fursa nzuri ya kubadilishana uzoefu na kuimarishana katika jukumu letu la msingi la kutoa huduma za hali ya hewa kwa ajili ya kulinda maisha ya watu na mali zao. Kwa upande wetu TMA tupo tayari kutoa uzoefu wetu wa kiutendaji na kuwajengea uwezo wataalamu wa hali ya hewa wa Zimbabwe ikiwemo katika Mifumo ya Udhibiti wa Ubora, Mifumo ya Utabiri wa Hali ya Hewa, Uchakataji na utunzaji wa tarifa za hali ya hewa, Uangazi wa Hali ya Hewa, na utoaji wa Huduma za Hali ya Hewa kwa sekta mbalimbali’. Alisisitiza Dkt. Chang’a





Aidha, kwa upande wa Mkurugenzi wa MSD - Zimbabwe, Bi. Rebecca Manzou, akiwasilisha salamu kutoka Zimbabwe, aliishukuru TMA kwa ukaribisho na mapokezi mazuri wakiwa na matumaini makubwa ya kujifunza namna TMA ilivyopiga hatua katika sekta ya hali ya hewa ikiwemo kuimarisha uchakataji na utunzaji wa takwimu za hali ya hewa na matumizi ya teknolojia za kisasa katika huduma za hali ya hewa.



TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

## FAHAMU ZAIDI


### HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MEI, 2025

Kipindi cha mwezi Juni 2025, maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa na hali ya baridi ya wastani hadi joto kiasi hadi. Hata hivyo, hali ya baridi ya wastani hadi baridi kali inatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Singida pamoja na maeneo ya magharibi mwa mkoa wa Dodoma. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa pwani, Ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki na nyanda za juu kusini magharibi. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ya ukanda wa pwani na maziwa makuu.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| **Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 ˚C hadi 25 ˚C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani na kati ya nyuzi joto 14 ˚C na 22 ˚C katika maeneo ya nchi kavu. Kwa ujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.** |
| **Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 ˚C hadi 18 ˚C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 12 ˚C. Kwa ujumla hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.** |
| **Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 ˚C hadi 20 ˚C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 14 ˚C. **Kwa upande mwingine, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.** |
| **Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 ˚C hadi 20 ˚C katika maeneo mengi. **Kwa upande mwingine, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.** |
| **Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 ˚C hadi 18 ˚C katika maeneo mengi. **Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| **Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 8 ˚C hadi 16 ˚C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko (ikijumuisha mkoa wa Njombe) yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 8 ˚C. **Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi na vipindi vichache vya mvua hususan katika maeneo yenye miinuko.** |
| **Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 ˚C hadi 24 ˚C katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.** |
| **Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 hadi 18 katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 10 katika kipindi cha mwezi Juni, 2025. **Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.** |

# MATUKIO KATIKA PICHA





*Wataalamu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kushirikiana na Benki ya CRDB kupitia mradi wa Tanzania Agriculture Climate Adaptation Technology Deployment Project (TACATDP) wakiwajengea uwezo Maafisa Ugani wa namna bora ya kutafsiri na kutumia taarifa za hali ya hewa hususani katika shughuli za kilimo mkoani Mbeya.*





*Baadhi ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) wakiwa katika kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa TMA kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa NSSF, Morogoro.*




**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Godfrey Kazinja

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa

www.meteo.go.tz
@tmaservices
@tma_servces
@tanzaniameteorological
www.meteotz1950.blogspot.com
tanzaniametagency
TMAonline_TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.